

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA
SHULE YA SEKONDARI SIKIRARI
S. L. P 155, SANYA JUU - SIHA

Kumb Na SKSS/JI/VOL2/09

Jina la Mwanafunzi _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SIKIRARI WILAYA YA SIHA, MKOA WA KILIMANJARO. MWAKA 2021

1.0. UTANGULIZI.

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika shule ya sekondari Sikirari Mwaka 2021. Shule ipo umbali wa km 1 karibu na Shule ya msingi Embukoi.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021 saa 1:15 asubuhi.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 SARE ZA SHULE.

- a) Wavulana suruali mbili (2) za kitambaa cha rangi ya zenye rinda mbili mbele, upana wa chini usiwe pungufu ya inchi 16 na Soksi pea 3 rangi NYEUSI
- b) Wasichana watashona sketi mbili za rinda box ambazo zitatakiwa kuvuka chini ya magoti kiasi cha urefu wa inchi 6 ya rangi ya na Soksi pea 3 rangi NYEUPE
- c) Kwa wote, Shati nyeupe ya mikono mifupi, Sweta rangi ya na viatu VYEUSI vya Ngozi visivyo na visigino virefu, pia ni lazima viwe vya kufunga Kamba.
- d) Wale wanaovaa hijabu wavae sketi ndefu, shati na hijabu nyeupe.
- e) Sare za michezo kwa shule hii ni bukta na T- shirt ya rangi ya BLUU na raba.

2.2 MAHITAJI YA DARASANI.

Madaftari counter books 2 quire 9 daftari ndogo 9 kwaajili ya majaribio ya kila wiki, mkebe wa hesabu, kalamu za kutosha, penseli, rula na vifutio.

2.3 HUDUMA YA CHAKULA.

Mzazi/Mlezi atahakikisha kuwa mtoto wake anapata huduma ya chakula shuleni kupitia kikao cha wazazi.

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya RAISI – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo msingi yafuatayo na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

- i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
- ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;

- iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
- iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ; na
- viii. Kutunza mali za umma.


3.1 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- i. Wizi.
- ii. Uasherati na Ushoga.
- iii. Ubakaji.
- iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- v. Kupigana au kupiga.
- vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
- vii. Kudharau Bendera ya Taifa.
- viii. Kuwa Mjamzito/ Kupata mimba.
- ix. Kuo au Kuolewa.
- x. Kutoa Mimba.
- xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- xii. Kukataa adhabu kwa makusudi.
- xiii. Kuwa na simu ya mkononi.

- 4.0. Mambo mengine Muhimu yanayopaswa kuwasilishwa shuleni na Mwanafunzi
- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospital ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
 - b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
 - c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheri, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

- 5.0. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

NB:- Kwa mzazi yeyote ambaye atampeleka mtoto wake shule ya binafsi alete uthibitisho kamili wa usajili wa mwanaye toka shule husika.

KARIBU SANA

 MKUU WA SHULE
 HEADMASTER
 SIKIRARI SECONDARY SCHOOL
 P.O. Box 155 SANYA JIJI